**Masomo ya Biblia**
**kwa ajili ya**
**KANISA LA ELOHIM (COG)**

**Siku Ya Saba (7th day)**

---

**Robo Ya Tatu**
**2016**

---

**KWA AJILI YA**
**Julai, Agosti, Septemba.**
**Kutumika na Biblia**

---

**Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

---

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**

**Jerusalem - Israel**

**--------------------------------------------------------**

**Somo Kwa Ajili Ya 2 Julai, 2016.**

## HALI ILIVYOTABIRIWA KATIKA SIKU ZA MWISHO

**Somo Kuu: 2 Timotheo 3**

**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 3:13.**

1. Ni hali gani au nyakati zipi kwa ujumla zitatawala katika "Siku za mwisho?" 2 Timotheo 3:1.
2. Tamaa na ubinafsi zitakuwaje katika nyakati za siku hizo? 2 Timotheo 3:2.
3. Watu watakuwa wapenda anasa katika kipindi hicho? 2 Timotheo 3:4.
4. Je, kutakuwa na watauwa wengi wa dini na wamasihi wajifanyao halisi? 2 Timotheo 3:5.
5. Kutakuwa na kujifunza kwingi kwa wakati huu, ni wengi wataufikia ujuzi wa kweli? 2 Timotheo 3:7.
6. Hali ya dunia itaendelea kuwa bora au mbaya zaidi baada ya mtume kutoa huu unabii? 2 Timotheo 3:13.
7. Mtume Yakobo anatujulisha nini kuhusu utajiri na mali katika siku za mwisho? Yakobo 5:1-3.
8. Isaya alitabiri nini kuhusu sheria na neno kutoka Yerusalemu katika siku za mwisho? Isaya 2:2, 3.
9. Naye nabii Mika pia alitabiri nini kuhusu tukio hili katika siku za mwisho? Mika 4:1, 2.

10. Kufuatia matukio haya, nini itafanyika huko Yerusalemu wakati Masihi atakaporudi kuleta hukumu? Mika 4:3.
11. Ni nini kilochosemwa kuhusu siku za mwisho au "wakati wa mwisho," kuhusu ongezeko la maarifa? Danieli 12:4.
12. Ni kwa muda gani Kitabu cha Danieli kitakuwa kimefungwa na kutiwa muhuri, na wakati kitafunguliwa wazi, nani atakuwa na hamu yake, nani ambaye hatakuwa na hamu yake? Danieli 12:9, 10.

**Kumbuka**: Kitabu cha Danieli bado kimefungwa na kutiwa muhuri kwa Israeli, na Wayahudi kwa ujumla. Laana imewekwa na Wayahudi waliokithiri (Orthodox Jews), juu ya mtu yeyote ambaye atakayetafsiri na kuhesabu Majuma 70 ya sura ya 9.
13. Nini kilichosemwa kuhusu njia za usafiri katika wakati wa maandalizi? Nahumu 2:3, 4.

**Kumbuka**: Tunaishi katika wakati wa maandalizi kwa ajili ya mfalme ajaye, na hali hizi zinadhihirika kila mahali. Kila mwanaume na mwanamke ambaye ameitwa kutoka dunia, na anaelewa mambo haya, lazima awe mtumishi mwenye faida na ushuhudiaji na kwa kujitolea maisha yake, katika zaka na sadaka, kuchapisha ujumbe huu, kuutuma kupitia wahudumu na wafanyakazi kwa Israeli, na kwa ulimwengu wa Wayunani.

******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 9 Julai 2016.**

**UNABII WA DANIELI**

**Somo Kuu: Danieli 9**
**Fungu La Kukariri: Danieli 9:22.**

1. Baada ya hekalu la Sulemani kuharibiwa, wana wa Israeli walichukuliwa mateka Babeli, lakini ni kwa muda gani walifaa kukaa huko? Yeremia 25: 10, 11.
2. Baada ya wao kukusanywa kutokana na mtawanyiko huu, nini ilifaa itendeke kwa Babeli? Yeremia 25: 12, 13.

**Kumbuka**: Ni ukweli unaojulikana, kulingana na maandiko na pia historia, kwamba Wayahudi walikusanywa tena Yerusalemu na hekalu lingine likajengwa mahali ambapo hekalu la Sulemani lilisimama.

3. Wakati Daniel alikuwa akiomba kwa ajili ya marejesho ya Israeli, nani ambaye alimtembelea? Danieli 9:20, 21.

4. Ni kwa kusudi gani Gabriel alimtembelea Danieli? Danieli 9:22, 23.
5. Ni kwa muda mngapi uliopeanwa kwa watu wa Israeli ili wafanye upatanisho kwa ajili ya dhambi na kufanya maridhiano kwa ajili ya uovu? Danieli 9:24.
6. Kuhusu adhabu ya Israeli, ni kipindi gani siku moja iliwakilisha? Ezekieli 4:5, 6.

**Kumbuka**: Kama ilivyoteuliwa kwa Israeli, siku moja kwa mwaka mmoja, wakati wa vipindi hivi vya adhabu, ni kwa kimantiki na maandiko kutumia kanuni hiyo kwa vipindi vya adhabu vitakavyofuata? Kwa hivyo kipindi hiki cha wiki 70 itakuwa 70 mara 7 au miaka 490, kwa sababu kuna siku saba katika wiki moja.

7. Gabriel alimpa Danieli hakikisho kwamba amri itatolewa kwenda kujenga Yerusalemu. Baada ya amri kutolewa, itakuwa kwa muda gani hata zamani zake Masihi? Danieli 9:25 [sehemu ya kwanza]
8. Yerusalemu ilikuwa ijengwe upya wakati wa amani au shida? Danieli 9:25[sehemu ya mwisho].
9. Nini ilikuwa itokee kwa Masihi baada ya majuma sitini na mawili pamoja na wiki saba za kwanza, kwa jumla wiki 69? Danieli 9:26 [sehemu ya kwanza].
10. Ni nani alikuwa afuate baada ya Masihi? Alikuwa afanye nini? Danieli 9:26 [sehemu ya mwisho].

**Kumbuka**: Huyu alikuwa Tito kamanda wa majeshi ya Kirumi ambaye aliuzingira mji wa Jerusalem katika mwaka wa 66 A.D, na kuharibu kabisa mji na hekalu la pili katika mwaka wa 70 A.D. Wale ambao walimpokea Yahshua, na kuamini maneno yake [Luka 21:20, 21] walikimbia kutoka mji. Kwa mujibu wa historia, majeshi ya Kirumi kwanza walizunguka Yerusalemu na kisha wakarudi kwa muda mfupi kabla ya kuuzingira kwenyewe. Wengi ambao walibaki katika mji walilia kwa kelele katika maombi wakimtafuta “Masihi wao aliyeahidiwa” ili awakomboe. Ni mpaka wakati wetu [karibu miaka 2000 baadaye] Wayahudi wameunganishwa tena na nchi yao.
11. Ni nini ilikuwa itokee katikati ya wiki hii ya mwisho ambayo ni wiki ya 70? Danieli 9:27 [sehemu ya kwanza].

**Kumbuka**: Hii ilikuwa kukatiliwa mbali, au kusulubiwa kwa Masihi, tukio ambalo lilileta rasmi mwisho, lengo na haja ya sheria ya msamaha kwa damu ya “kondoo la dhabihu” na kuleta kipindi kipya cha neema.
12. Nini ilikuwa itokee baada ya kusulubiwa, kuhusiana na chukizo la uharibifu? Danieli 9:27 [sehemu ya mwisho]. Mwisho wa ukiwa ulikuwa hadi lini?

**Kumbuka**: Kama Masihi hajakuja tayari kulingana na Danieli 9:26, Israeli haingekuwa hapa kuishi na Yerusalemu ingeondolewa tena na kuharibiwa. Baadhi miongoni mwa Wayahudi wa kidini, wanaoishi katika Israeli leo, hawaitambui nchi ya Israeli kwa sababu ya unabii huu. Hawaelewi ya kwamba unabii huu ulitimizwa wakati Yahshua alipokuja na katika miaka ya karibuni iliyofuatia, katika karne ya kwanza hii upande wa Masihi; kwamba Yahshua ni Masihi; kwa hivyo Israeli iko hapa kuishi; na Israeli leo hii ni utimilifu

wa moja kwa moja wa unabii mzuri na wa kudumu ambao Wayahudi wamekuwa daima wakiuombea na kungoja kwa muda mrefu. [Nyakati na vipindi ni kamili].

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 16 Julai, 2016.**

**WITO NA USHUHUDIAJI WA MITUME**

**Somo Kuu: Matthew 10 sura.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 10:16.**

1. Ni nguvu ipi waliopewa Mitume? Mathayo 10:5-8.
2. Ni maagizo yapi ya kiujumla yalitolewa? Mathayo 10:9-16.
3. Yahshua aliwaambia nini kuhusu upinzani watakaokutana nao? Mathayo 10:17-31.

**Kumbuka**: Wavuvi hawa wasio na masomo na wasio na ujasiri kutoka Galilaya, wanaume wachache wadhaifu, walitumwa dhidi ya nguvu zote za Mataifa. Kutokana na haya kazi yao ilikuwa haiwezekani, lakini uwezo wa Mbinguni ulikuwa pamoja nao, na ahadi hiyo pia ni yetu leo, "... Tazama, mimi nipo pamoja nanyi daima, hata mwisho wa dunia. Amina." (Mathayo. 28: 20.)

4. Ni ahadi gani Mwokozi alipeana? Mathayo 10:32-39.

**Kumbuka**: Kuna njia nyingi za kumkana: kwa kusema maovu, na kufuata anasa za dhambi, na kukataa dhabihu na kujikana binafsi kwa ajilli yake, na kazi yake, na kwa kuwa na maoni yetu wenyewe kuyapinga maneno yake.

5. Je, tendo ndogo jema letu laonekana vipi kwa Bwana? Mathayo 10:40-42.
6. Wakati Mitume waliporudi kutoka ziara yao ya kuhubiri walifanya nini na ni wapi wao walienda na kwa nini? Marko 6:30-32.
7. Ni mwaliko upi wa upendo na ahadi Yahshua awaitia wale waliolemewa na kusumbuka? Mathayo 11:28-30.
8. Ni muujiza upi wa ajabu, alitenda kuonyesha nguvu ambayo aliyokuwa nayo? Marko5:1, 8, 15.
9. Wakati mtu huyu alitaka kuandamana na Bwana, alimwambia huyo mtu ajitahidi kufanya nini? Marko 5:18-20.
10. Hali ya mtu mwingine aliyeletwa mbele ya Yahshua ilikuwa vipi, na matokeo yalikuwa yapi? Mathayo 12:22, 23.

**Kumbuka**: Hii ilikuwa kazi ya Mwokozi wetu, ambayo aliyoikabidhi kwa wawakilishi wake. Alielewa sheria takatifu ya mbinguni kwamba dhambi ni shina la maovu kama hayo, ambayo yeye aliyashambulia kwanza. Kazi yake ilikuwa kuweka asili ya binadamu huru kutokana na maovu yake mengi, kwa kutenda juu ya chanzo. Huruma yake na huruma ya kina kwa ajili ya wanaoteseka kulileta machozi kwa macho yake, huruma kila mara iliambatana na uweza.

11. Jinsi gani alijibu mashtaka yaliyotolewa na Mafarisayo? Mathayo 12:24-30; Luka 11:15-23.

**Kumbuka**: Baba wa Mbinguni hutumia watu mwanga, kwamba njia zao mbaya ziweze kurekebishwa, lakini wakati muale mmoja wa nuru unakataliwa, mtazamo wa kiroho unaathiriwa kiasi, na kufunuliwa kwa nuru mara ya pili kunaeleweka kidogo. Kisha giza huongezeka polepole na kukaa.

12. Ni onyo gani alitoa kuhusu kukataa nuru, na kunena neno juu ya Roho Mtakatifu? Mathayo 12:31-32; 2 Wathesalonike 2:10-12.

13. Nini kilichosemwa kuhusu maneno mabaya, maneno mazuri, na pia maneno yetu katika siku ya hukumu? Mathayo 12:34-37.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 23 Julai, 2016.**

## ADHABU YA ISRAELI

**Somo Kuu: Walawi 23:1-31**
**Fungu La Kukariri: Luka 21:24.**

1. Ni baraka na ulinzi upi waliahidiwa Israeli kama watamtii Bwana? Mambo ya Walawi 26: 3-12.
2. Ikiwa walishindwa kutii, ni nini itakuwa adhabu yao? Mambo ya Walawi 6:14-17.
3. Ni kwa muda gani wao wataendelea kuadhibiwa? Mambo ya Walawi 26:18.
4. Ni nini inaonyesha ukali wa hukumu ya Elohim juu yao? Mambo ya Walawi 26:19, 21, 24, 28.

**Kumbuka**: Matumizi mengi ya usemi “mara saba” haina maana mara kadhaa saba. “Saba” katika maandiko inamaanisha ukamilifu; kwa hivyo, hii hutumika kutilia mkazo kuelezea ukamilifu wa adhabu yao. Mara saba kwa siku kwa mwaka au miaka 2520, ilianza na utumwa wa Babeli chini ya Nebukadreza 606 B.C., na kumalizika na uhamishaji wa Waturuki katika Palestina chini ya Allenby mkuu katika vita kuu vya dunia mara ya kwanza, mwaka 1914.

5. Watika wa miaka hii, ni nini kilichonenwa kuhusu nchi yao? Mambo ya Walawi 26: 31-35.
6. Hii adhabu kali itawasababisha kufanya nini? Mambo ya Walawi 26: 28, 29.
7. Ni maelezo mengine yapi yametumiwa kuonyesha ukali wa adhabu yao? Yeremia 31:27, 28
8. Wakati wa hii miaka ya utumwa, jinsi gani walisimama mbele ya Elohim? Yeremia 31:35-37.

9. Ni nini kilichosemwa kuhusu kujulikana kwao kati ya mataifa wakati huu? Isaya 61: 9.
10. Lengo halisi juu ya mateso haya ni nini? Hosea 5:15.
11. kwa nini Elohim hangewaangamiza kabisa wakati wa miaka hii? Mambo ya Walawi 26:44, 45
12. Ni unabii upi wa Daudi huwa unatimia sasa? Zaburi 102:15, 16

******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 30 Julai, 2016.**

**USHINDI WA YAHSHUA JUU YA MAJARIBU**

**Somo Kuu: Mathayo 4:1-11**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 4:5**

1. Wakati Yahshua alibatizwa katika mto Yordani, ni nini kilichotokea huko katika mto kumwezesha yeye zaidi? Mathayo 3:16, 17; Luka 3:21, 22.
2. Ni jaribu lipi la kwanza ibilisi alimtolea Yahshua? Mathayo 4:1-3.

**Kumbuka**: Shetani daima anamjaribu mtu katika moja ya hali dhaifu na juu ya kiwango chake dhaifu. Sisi ni lazima tuimarike vizuri kwa ukweli wa Biblia kama tutasimama imara dhidi ya mapendekezo na uongo wa Shetani.
3. Yahshua alijibuje mbele ya Shetani kwa majaribu yake? Mstari wa 4.
4. Eleza majaribu ya pili kwa Masihi? Mathayo 4:5, 6.
5. Katika hayo yote alikuta nayo, jinsi gani Yahshua alimweza adui? Yeye alitumia hekima au falsafa ya mtu kupambana na majaribu? Mstari wa 7.

**Kumbuka**: Utatambua kwamba Shetani alinukuu maandiko katika kumjaribu Yahshua. Yahshua alikuwa na maarifa ya kina sana ya neno na mapenzi ya Baba wa mbinguni. Katika siku hizi za udanganyifu tunahitaji kuwa makini na kujaribu kila Roho kwa neno la Elohim. Katika kujitolea kujifunza neno, ni muhimu sana kwamba tuweza kuomba kwa ajili ya upendo safi na mkuu wa kweli, kwani kuna wengine “milele hujifunza, na kamwe hawana uwezo wa kufahamu ukweli,” 2 Timotheo 3:7, na wengi huyapotoa maandiko kwa uharibifu wao wenyewe. 2 Petro 3:16. Kwa wale upenda haki watakuwa wazi kufikiri bila kuwa na mawazo wanayoyapendelea wao wenyewe. Ni sharti kutokuwa na wazo lolote ndani yetu linalotoka akilini mwetu au imani ya mtu]. Yote lazima “yapitishwe kwa Elohim,” 2 Timotheo 2:15. Kwa upande wa wanadamu, pia, lazima kuwe hakuna kuchafuliwa kwa neno. Tafadhali soma 2 Wakorintho 2:17; 4:2; Yohana 10:27; 17:17; Warumi 3:4.

6. Ni toleo gani la kilele ibilisi alitoa katika juhudi zake za mwisho kumjaribu Yahshua? Jinsi gani yeye alikemewa? Mathayo 4:8-11.

**Kumbuka**: Katika kulinganisha kujaribiwa kwa Yahshua na toleo la kumjaribu Hawa, ni jambo la kustusha kuona jinsi hayo majaribu yalivyo sawa. Tamaa zilizotajwa katika 1 Yohana 2:15-17, "tamaa za mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha maisha," zilitumika na Shetani katika mifano yote miwili. Mtu wa kwanza, Adamu, akaanguka, lakini Adamu wa pili alishinda, na kupitia ushindi wake sisi pia tunaweza kushinda. 1 Wakorintho 15:22, 45.

7. Tumehimizwa kufanya nini ili tuweze kuishi maisha ya ushindi na ya manufaa? Waebrania 4:4-16.

******************************

**Somo Kwa Ajili Ya Agosti 6, 2016.**

**UTAJIRI WA MILELE**

**Somo Kuu: 1 Timotheo 6**
**Fungu La Kukariri: 1 Timotheo 6:11.**

1. Ni nini mada ya mahubiri ya Paulo kuhusu utajiri, katika Waefeso 3:8 na ni maonyo yametolewa katika 1 Timotheo 6:17-19?
2. Ni hali gani halisi ya wengi ambao ni maskini katika mali ya kidunia na ya hao wengine walio matajiri? Ufunuo 2:9, 3:15-17.
3. Ili kushiriki utajiri usiopimika, ni maelekezo gani zaidi yamepeanwa katika Ufunuo 3:18?
4. Ni nani ambaye anasimama mlangoni, tayari kila wakati kutusaidia? Ufunuo 3:20.
5. Ikiwa sisi kupitia uwepo na msaada wake, tuna mafanikio katika kushinda ulimwengu na vivutio vyake, ni ahadi gani Yahshua ametuahidia kwa ajili ya hayo? Revelation 3:21.
6. Ingawa Yahshua mwenyewe alikuwa maskini hivyo kwamba hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake, Je, yeye anamiliki uwezo wa kupeana utajiri halisi kwa wengine, na yeye hajafanya hivyo? 2 Wakorintho 6:10.
7. Ni onyo lipi limetolewa kuhusu tamaa na uzima wa mtu kweli umo katika vitu ambavyo alivyo navyo yeye? Luka 12:15.
8. Imesemekana vipi kuhusu mtu ambaye amejiwekea hazina za kidunia na si tajiri kwa Elohim? Luka 12:16-21.

**Kumbuka**: Masihi hajashutumu hazina za kidunia bora mtu huyo awe tajiri kwa Elohim na kugawanya naye sehemu inayohitajika, na katika kufanya hivyo pia kuwasaidia wale walio na mahitaji.

9. Watu waaminifu wa Bwana wanafaa kuacha ukarimu wa kusaidiana na fedha zao kwa hofu kwamba waweza kuja kuhitaji na kuteseka? Luka 12:22-30.
10. Jinsi gani tutaweka hazina za kidunia katika akiba ya mbinguni? Luka 12:31, 33, 34.
11. Ni nini kilichosemwa kuhusu taa zetu kuwaka na pia kuwa tayari kukutana na Bwana wakati atakapokuja? Luka 12; 35, 36.

**Kumbuka**: Yahshua alisema kwamba amewachagua maskini wa dunia hii, wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme, na hivyo maneno yake ni ya kweli hadi wa leo. Maskini ni watu ambao daima hukubali kwa haraka zaidi ujumbe wa injili katika nyanja zote za kazi.

******************************

**Somo Kwa Ajili Ya Agosti 13, 2016.**

## ULIMI USIOFUGIKA

**Somo Kuu: Yakobo 3**
**Fungu La Kukariri: Yakobo 3:2**

1. Katika Zaburi 34:13 tunaambiwa tuzuie ndimi zetu kutokana na nini?
2. Ni mfano gani mfalme Daudi alitupa katika Zaburi 35:28?
3. Tunafaa kuwa na maombi gani kuhusu ulimi? Zaburi 120:2.
4. Kinywa cha mwenye haki hutoa nini? Mithali 10:31.
5. Ni nini lazima kila ulimi wafaa kukiri? Warumi 14:11; Wafilipi 2:11.
6. Je, Yakobo 1:26 inatuambia nini kuhusu MMasihi ambaye hawezi kuzuia ulimi wake?
7. Tumeonywa vipi kuhusu ulimi na moto? Yakobo 3:5.
8. Ni ushauri upi, Petro anatoa kwetu kuhusu tabia zetu na ulimi? 1 Petro 3:10.
9. Jinsi gani tunapaswa kuongea kuhusu mwanadamu mwenzetu? Tito 3:2.

******************************

**Somo Kwa Ajili Ya Agosti 20, 2016.**

## KUZALIWA KWA YAHSHUA

Maandiko matakatifu yanatueleza kwamba Masihi ni wa "nyota ya Yakobo" (Hesabu 24:17); "Nyota ya siku" (2 Petro 1:19); "Nyota yenye kung’aa ya asubuhi" (Ufunuo 22:16). Mamajusi kutoka Mashariki walikuwa si wataalamu wa nyota tu kama baadhi ya watu ufundisha. Waliona "Nyota" na wakaamua "kuja kumwabudu."

Tunaamini walikuja kwa kuongozwa na Elohim, "kwa maana dunia kwa hekima haikumjua Elohim.", 1 Wakorintho 1:21.

**Somo Kuu: Mathayo 1:18-25.**
**Mistari ya kumbukumbu: Luka 2:13, 14.**

1. Lengo la safari ya Joseph na Maria kwenda Bethlehemu lilikuwa lipi? Luka 2:1-5.
2. Wakiwa huko Bethlehemu, ni tukio gani la ajabu lilitokea? Luka 2:6, 7.
3. Ni nini kilichosemwa juu ya wachungaji wakati huu? Luka 2:8.
4. Ni utukufu gani wao waliruhusiwa kutazama? Luka 2:9.
5. Ni ujumbe gani wa ajabu malaika waliwapa? Luka 2:10, 11.
6. Ni ishara gani walipewa kuhusu mtoto huyu? Luka 2:12.
7. Ni habari nyingine zipi za utukufu walizopokea wachungaji? Luka 2:13, 14.
8. Wakati malaika waliondoka, ni nini wachungaji waliamua kufanya? Luka 2:15.
9. Wakati walifika mahali paliponenwa na malaika, waliona nini? Luka 2:16.
10. Wachungaji walifanya nini kuhusu habari njema waliopokea? Luka 2:17.
11. Jinsi gani wasikilizaji waliichukua ripoti hiyo? Luka 2:18.
12. Mtazamo wa Maria kuhusu tukio hili ulikuwa upi? Luka 2:19.
13. Jinsi gani wachungaji walidhihirisha furaha yao kwa ajili ya Mwokozi? Luka 2:20.
14. Wakati huyu mtoto alipotimia umri wa siku nane, walifanya nini kulingana na sheria na yeye aliitwa jina lipi? Luka 2:21 (sehemu ya kwanza).
15. Ni kwa kupitia nani alipewa hilo jina lake kabla hajachukuliwa mimba? Luka 2:21(Sehemu ya mwisho).
16. Nani alikuwa mfalme wa Yudea wakati huu? Ambaye pia alikuja Yerusalemu? Mathayo 2:1.
17. Maswali yao yalikuwa aje? Ni sababu gani wao walizotoa kwa ajili ya kuja? Mathayo 2:2.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya Agosti 27, 2016.**

**INJILI YA UFALME**

**Somo Kuu: Mathayo 9:35-38.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 9:35.**

1. Ni mfano gani Masihi alitupa kuhusu injili? Mathayo 9:35, soma pia Marko 1:14.
2. Ni ishara gani Mwokozi alitoa kwake Yohana kuonyesha kwamba yeye ndiye Masihi? Luka 7:22.
3. Masihi alitoa amri gani kwa wale ambao wamfuatao? Marko 16:15.

4. Ni wizara gani Mitume walipokea kutoka kwa Mwokozi? Matendo ya Mitume 20:20-24.
5. Tumetumwa kuhubiri injili? Warumi 10:15.
6. Je, ni muhimu kiasi gani kuhubiri injili? 1 Wakorintho 9:16.
7. Ni kwa nani injili lazima ihubiriwe, na ni kwa nguvu gani huwa twahubiri injili? Warumi 1:16.
8. Ni injili gani lazima ihubiriwe kwanza kabla ya Masihi kurudi? Mathayo 24:14, soma pia Marko 13:10.
9. Tumeambiwa ni nini kitatokea kwa mtu yeyote atakayehubiri Injili nyingine? Wagalatia 1:9.

**Kumbuka**: Ni baraka kuwa mtumishi wa injili. Biblia inatuambia kwamba Baba anapenda watoto wake wote wamjue yeye, kwa hiyo yeye ametutuma sisi kuhubiri injili ya ufalme kwa kila taifa, na kwa watu wote. Hebu tuubebe huu ukweli kwa imani isiyotingika, na tuwe tayari wakati wote ili kumtumikia yeye.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 3 Septemba, 2016.**

**KUJUMUISHWA KWA WAYUNANI KATIKA JAMII YA ISRAELI**

**Somo Kuu: Warumi 11; Waefeso 2.**
**Mistari ya kumbukumbu: Waefeso 2:12, 13.**

1. Wayahudi walikuwa na ziada gani juu ya mataifa mengine chini ya mbingu? Warumi 3:1, 2; 3:9:4, 5; Yohana 4:22.
2. Je, Biblia inasemaje juu ya Mataifa? Waefeso 2:12.
3. Nii ahadi gani isiyo na dosari Elohim huwapa? Hosea 2:23; Isaya 62:2.
4. Katika utekelezaji wa ahadi yake kwa Mataifa, hali gani mbaya iliangukia taifa la Kiyahudi? Warumi 11:7-10.
5. Hali hiyo itawakumba hata lini? Isaya 6:11-13.
6. Ni matokeo yapi ya ajabu kutokana na kuanguka kwa taifa la Kiyahudi yako kwenye mataifa ya Wayunani? Warumi 11:11, 25, 28, 30-33.
7. Ni nini imewezesha mataifa ya Wayunani kupandikizwa katika jamii ya Israeli? Waefeso 2:11-14.
8. Wao sasa ni washiriki wa familia ya Ibrahimu na warithi? Wagalatia 3:26-29; Waefeso 3:5, 6; Warumi 10:12.
9. Ni onyo gani kali imetolewa kwa warithi wa kupandikizwa? Warumi 11:20-23.
10. Je, Mataifa waumini wanatarajiwa kufanya nini? 1 Petro 2:5, 9, 10.
11. Ni kwa njia gani hili tendo la ajabu la Elohim halichunguziki? Warumi 11:33-36.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 10 Septemba, 2016.**

**MABAKI YA WAUMINI WANA KAZI YA KUFANYA**

**Somo Kuu: Yohana 15**

**Fungu La Kukariri: Yohana 15:8**

1. Kila mtumishi mwaminifu amepewa kitu cha kufanya? Marko 13:34.
2. Ni kitu gani kingine kimetolewa kwa wanafunzi wake? Mathayo 25: 15.
3. Kwa hivyo wanafunzi pia huitwa vipi, ambao wamepewa kazi? Mathayo 25: 14.
4. Ni nini kinatokea kwa kila mmoja ambaye anashindwa katika usimamizi wake kuleta nyongesa kwa ufalme? Yohana 15:2.
5. Ni muhimu kuwa na uhusiano wowote maalum na mbinguni, kwa ajili ya uwepo wa kudumu wa Roho? Yohana 15:4, 5.
6. Je, ni mahitaji gani maalum tunahitaji ili maombi yetu yasikike na yajibiwe? Yohana 15:16.
7. Ni nini kitatokea kwa wanafunzi wote ambao wanaishi tu kwa nguvu zao wenyewe na hawakai daima katika Masihi? Yohana 15:6.

**Kumbuka**: Nguvu ya injili ambayo huleta uthibitisho kwenye moyo wa mwenye dhambi, na inatoa ushindi kwa mtumishi juu yake mwenyewe, inapeanwa tu kupitia mawasiliano ya mara kwa mara na Mwokozi kupitia kwa maombi. Kuacha kuomba ni kama kutoa waya ya jenereta kwenye gari lako. Nuru yako itapungua hivi karibuni, na hatimaye kuzimika.

8. Ahadi gani imetolewa kwa wale watapanda mbegu ya injili? Zaburi 126:5, 6
9. Ni ahadi gani kwa yule atakayevuta roho za watu? Mithali 11:30; Danieli 12:3.
10. Licha ya kuonyesha wenye dhambi kuhusu makosa ya njia zao, na kuwavuta wao kwa ufalme, ni kazi gani nyingine tumepewa kufanya? Mithali 19:17; Isaya 1:17.
11. Ni nini kilichosemwa kuhusu wale ambao wataziba masikio yao wasisikie kilio cha maskini? Mithali 21:13.
12. Ni nini imetangazwa kuwa dini iliyo safi? Yakobo 1:27.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 17 Septemba, 2016.**

**AMBAYE BWANA AMPENDA HUMRUDI**

**Somo Kuu: Waebrania 12:1-13**

**Fungu La Kukariri: Waebrania 12:7**

1. Jinsi gani Elohim hushughulikia wale anaowapenda? Waebrania 12:5.

2. Elohim atatuona vipi kama tutafaidika na kurudiwa? Waebrania 12:6-9.

3. Lengo la Elohim katika kurekebisha watu wake ni lipi? Waebrania 12:10, 11.

**Kumbuka**: Adhabu ya Bwana ni kama moto unaotakasa dhahabu, miali ya usahihishaji itatuchoma na kuondoa uovu wote katika maisha yetu ikiwa tutamruhusu kufanya kazi yake ndani yetu.

4. Wakati tumeadhibiwa yafaa tufanye nini? Ufunuo 3:19.

5 Mfano gani bora wa mtu kwa Biblia aliyefaidika na adhabu? Yona 1:1.

6. Ni kazi gani alikuwa afanye, na yeye alifanya nini? Yona 1:2, 3.

7. Elohim alikabiliana na huyu mtu jinsi gani? Yona 1:17. Matokeo yalikuwa yapi? Yona 3:3, 5.

8. Sauli alikuwa na uzoefu gani sawa? Matendo ya Mitume 9:1-4.

9. Alielekezwa kuuliza nini? Matendo ya Mitume 9:5, 6.

**Kumbuka**: Bila shaka Sauli, ambaye alikuwa mtu mwaminifu hata kabla ya uongofu wake, hakuweza kuelewa kwa huo wakati kwa nini mkono wa Elohim ulikuwa juu yake. Basi leo hatuwezi kujua kwa nini majaribu yanakuja au matarajio yetu kukatishwa, bado kwa imani tunajua Masihi ni kutuandaa kama vyombo vya dhamana ilitung'ae katika ufalme wake.

10. Katika siku za mwisho za Paulo, ni maneno gani mazuri alikuwa na uwezo wa kusema? 2 Timotheo 4:6-8.

11. Dhiki uongoza walio wa kweli wapi? Warumi 5:3-5.

12. Kwa kuishi karibu na Yahshua, Paulo alisema nini? 2 Wakorintho 7:4.

**Kumbuka**: Kuwa na furaha sana katika dhiki ilikuwa ushuhuda ambao Paulo angeweza kutoa. Alitoka mbali sana kupitia uzoefu wake wa KiMasihi tangu alipokutana na Masihi njiani akielekea Damaski, na alijifunza, kwa kupitia mateso yake na matatizo, masomo ya thamani ya kiroho ambayo yawanufaisha watoto wa Elohim hata leo.

*******************************

**Somo Kwa Ajili Ya 24 Septemba, 2016.**

**MBEGU ILIYOTEULIWA**

**Somo Kuu: Isaya 60**

**Fungu La Kukariri: Isaya 60:21.**

1. Ni ahadi gani iliyofanywa kwa uzao wa Ibrahimu, na kwa nini? Mwanzo 22:17; 26:5.

2. Ni kwa umbali gani baraka za Ibrahimu zilifaa kufika? Wengine pia walikuwa wabarikiwe kupitia uzao wake? Mwanzo 12:2, 3; 22:18; 26: 4.
3. Israeli daima alikuwa mwaminifu kwa tumaini lililotolewa kwao? Yeremia 2:21, 22; Mambo ya Walawi 26: 33; Nehemia 13:17, 18; Ezekieli 6:8; 22:4, 14, 15.

**Kumbuka**: Kuna somo rahisi hapa, kwa ajili ya sisi sote kujifunza, kuhusu wakati wa kutawanywa kwa Israeli. Kama Andrew Dugger (mpendwa Baba yetu na Mzee wa kanisa) alivyosema, "Wayahudi ni ushuhuda hai wa ghadhabu ya Elohim juu ya wana wa uasi." Tafadhali soma Warumi 11:21.
4. Katika kugusia nguvu upendo, huruma na Urejesho wa Elohim, Je, neno la Elohim lazidi kutuambia nini kuhusu familia ya Kiibrahimu? Isaya 61:3, 4; 49: 12-16; 48: 9-12; Yeremia 31:7-12; 31:35-37; Ezekieli 36: 8-11.
5. Je, Elohim bado ana kusudi la kuhifadhi uzao wa Israeli? Isaya 2:2; 49:6-11; 59:19-21; 60: 1-3; 62: 1-7; Mika 4:1, 2; Luka 1:31-33.
6. Wayunani watabarikiwa kwa njia gani kupitia familia hii iliyochaguliwa? Matendo 3:22-25;Waefeso 2:12-14; Wagalatia 3:29; Yohana 4:22; 18:37; Mathayo 2:2; Luka 2:14; Isaya 9:6, 7; Ufunuo 5:9, 10.

**Kumbuka**: Ahadi zaidi za kinabii (chache tu kati ya nyingi) walitabiri nyakati bora kwa Israeli, zapatikana katika Zekaria 8:1-8; Ezekiel 36: 25.. Mbingu iliamuru kwamba Jerusalem itaneemeshwa tena. Sisi ni mashahidi wa kwanza wa ukweli huu. Unabii mwingi wa kale nimtimilifu leo hii. Elohim bado anaongoza Israeli na ahadi zote zitakamilika. Yeye anafanya kazi kwa kusudi lake kupitia Israeli.
7. Je, ni ishara gani ya uhakika zaidi na bora ya Mwokozi wetu ya kurudi hivi karibuni, iliyotajwa katika Biblia na pia hupatikana katika Zaburi nzuri sura ya 102? Mstari wa 16.
8. Ni hali gani maalum sana iliyotabiriwa katika unabii kwa watu wake kabla ya kuja kwake kwa mara ya pili? Isaya 52:8.

**Kumbuka**: Uhalisi wa neno la Elohim na hata uwepo wa Elohim umehalalishwa kupitia Israeli. Ni kama ilivyokuwa wakati wa mwanzo sana neno liliposikika na kwa neno lake vitu vizuri viliumbwa - hata sasa, amenena kuhusu Israeli nyakati za leo. Kupitia ya kale, na katika wakati huu, hadi mambo yote ya baadaye, neno lake litaendelea kufunuliwa - kamili kwa kila amri. Katika nyakati hizi ngumu mno, tumepokea faraja kwa sababu tunajua kwamba neno lake ni la kweli na kwamba yeye ana udhibiti.

9. Katika siku zijazo, wakati mataifa watakuja dhidi ya Yerusalemu, nani ambao watakuwa wanaishi katika nchi ya ahadi? Itakuwa ni uzao halisi wa Israeli, au ni watu wa Mataifa? Ezekieli 38:16.

******************************